


Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 04 Issue: 01 | February-2026

EAJK

# Mchango wa Miktadha ya kijamii katika Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Pili Nchini Burundi

**Authors**

**Consolée Kamaro [(1)]; Rajabu Chipila [(2)]**

**Main author's email: kamaroconsolee73@gmail.com**

**(1) Burundi Higher Institute of Education, Burundi; (2) University of Dar es Salaam, Tanzania.**

**Cite this article in APA**

Kamaro, C., & Chipila, R. (2026). Mchango wa miktadha ya kijamii katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili nchini Burundi. *East Africa journal of Kiswahili*, 4(1), 11-23. https://doi.org/10.51317/eajk.v5i1.884

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 2025-12-15
Accepted: 2026-01-10
Published: 2026-02-09

**Scan this QR to read the paper online**

**Copyright**: ©2026 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).

**Ikisiri**

Makala hii inahusu miktadha ya kijamii na mchango wake katika kujifunza Kiswahili kama lugha ya pili nchini Burundi. Utafiti huu ulifanyika Nchini Burundi, Mkoa wa Bujumbura, katika Tarafa za Mukaza na Ntahangwa. Kimahususi zaidi utafiti huu ulifanyika katika vyuo vikuu vya serikali ambavyo vina idara za Kiswahili yaani Chuo Kikuu cha Ualimu (ENS) na Chuo Kikuu cha Burundi (UB). Nadharia ya Mwingiliano Jamii iliyoasisiwa na Mwanasaikolojia Vygotsky (1978) iliongoza utafiti huu. Utafiti huu ulitumia sampuli ya wasailiwa ishirini (20) wa kiwango cha shahada ya awali, mwaka wa tatu. Sampuli tajwa ilipatikana kwa usampulishaji nasibu sahili. Ukusanyaji wa data uliwezeshwa na mbinu ya usaili. Mikabala ya kitaamuli na kitakwimu na mbinu ya uchanganuzi wa data kimaelezo imetumika katika uchanganuzi wa data za utafiti huu. Data za utafiti huu zimewasilishwa kwa kutumia majedwali na grafu zilizoambatana na maelezo kwa ajili ya kutoa ufafanuzi zaidi. Matokeo ya utafiti huu yamebainisha kuwa miktadha ya kijamii ya kujifunza Kiswahili jijini Bujumbura ni soko, hospitali, zahanati, nyumbani, na kadhalika. Matokeo pia yalionesha kuwa miktadha hiyo inawawezesha wanafunzi kuingiza msamiati mpya, kukuza stadi za kusikiliza na kuzungumza. Inawawezesha pia, kuimarisha umilisi wa utamaduni na maarifa kuhusu fasihi. Mwisho, makala hii inapendekeza serikali ya Burundi iwezeshe walimu wa Kiswahili kufuatilia ujifunzaji wa Kiswahili wa wanafunzi nje ya darasa.

**Maneno Muhimu:** Lugha ya pili, lugha, miktadha ya kijamii, ujifunzaji, wanafunzi.

## 1.0 UTANGULIZI

Makala hii imelenga kubainisha miktadha ya Kiswahili ya kijamii na umuhimu wake katika kujifunza Kiswahili kama lugha ya pili (kuanzia sasa L2) nchini Burundi. Miktadha ya kijamii huhusisha mambo yote yanayoihusu jamii. Baadhi ya mambo hayo ni lugha, utamaduni, utawala, historia, uchumi, na kadhalika. Mikakati hii humpatia nafasi mwanafunzi kutoa mawazo na hisia zake juu ya mambo yanayoizunguka jamii hiyo. Hivyo humwezesha mwanafunzi kujifunza lugha, utamaduni na fasihi ya jamii hiyo kwa upesi zaidi kutokana na ushirikiano mkubwa wa wanajamii. Miktadha ya kijamii huathiri ujifunzaji wa lugha ya pili kwa kuchochea mawasiliano ya kuongea, kukuza, na kuboresha matumizi halisi ya lugha katika mazingira ya kawaida (Ellis, 2008). Hali hii ilimchochea mtafiti kufanya utafiti huu ili kubainisha miktadha ya kijamii iliyopo jijini Bujumbura na kuonesha mchango wake katika kujifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Utafiti huu ulijikita katika miktadha ya kijami kwa sababu miktadha hiyo inakwenda sambamba na mbinu za kujifunza lugha kwa wazungumzaji wa lugha ndani ya jamii. Hivyo, miktadha ya kijamii imeonesha matokeo mazuri katika kujifunza hususan kuimarisha stadi za kusikiliza na kuzungumza. Kwa mujibu wa Long (1996) na Gass (1997), mjifunzaji wa lugha akitangamana na wazungumzaji wa lugha hiyo anapata fursa ya kukuza stadi za kusikiliza na kuzungumza lugha husika.

Lugha ni chombo cha mawasiliano ambacho binadamu hutumia kuwasilisha ujumbe kwa binadamu wengine. Hivyo basi, lugha haiwezi kutenganishwa na jamii. Muundo wa kijamii huamua lugha na tabia ya wanajamii (Wardhaugh, 2006). Tafiti zinaonesha kuwa vigeu vya kijamii vinaathiri upataji wa lugha na mchakato wake wa ujifunzaji. Kwa mfano, Labov (2000) alieleza kuwa hali ya jamii huathiri msamiati na matamshi katika ujifunzaji wa L2. Pia, tafiti mbalimbali zinaeleza kuwa, matukio ya hali ya kijamii na kiuchumi ya wanafunzi yanaathiri ujifunzaji wao wa L2. Basi, jamii ambapo wanafunzi huishi, hushawishi zaidi ujifunzaji wa lugha (Stern, 1983).

Katika muktadha wa kitaifa wa Burundi, ambapo lugha za Kirundi, Kifaransa, Kiingereza na Kiswahili hutumika katika nyanja mbalimbali za kijamii, kiutawala na kiuchumi, ujifunzaji wa Kiswahili kama L2 unaanza kushika kasi. Kiswahili kilipata nafasi ya kipekee katika Jumuia ya Afrika Mashariki, ambako Burundi ni mwanachama, na hivyo kukifanya kuwa lugha muhimu ya mawasiliano ya kikanda, kibiashara na kidiplomasia. Licha ya hayo, changamoto za ujifunzaji wake bado zipo, hasa kwa wanafunzi wa vyuo vikuu ambao mara nyingi hukosa mazingira halisi ya matumizi ya lugha hiyo. Katika mazingira haya, miktadha ya kijamii kama vile hospitalini, vyombo vya habari, familia, kanisa na sokoni, huibuka na kuwa nyenzo muhimu inayoweza kuchangia uelewa wa matumizi ya Kiswahili.

Aidha kutokana na mchango wake katika kuimarisha ujumuishaji wa kikanda, serikali ya Burundi iliamua kufundisha Kiswahili tangu shule za msingi hadi vyuo vikuu. Hali hii inathibitisha kuwa kujifunza Kiswahili si tu hitaji la kitaaluma, bali pia ni mahitaji halisi ya kijamii na kiuchumi kwa Warundi wengi. Utafiti huu umelenga kuchunguza namna miktadha hiyo inavyoweza kuimarisha upataji wa umahiri wa Kiswahili kama L2 kwa kuzingatia hali halisi ya jamii ya Burundi.

## 2.0 NADHARIA YA UTAFITI

Wataalamu wamejadili nadharia mbalimbali juu ya kufundisha na kujifunza L2. Baadhi ya nadharia hizo ni Nadharia ya Mwingiliano Jamii iliyoasisiwa na mwanasaikolojia Vygotsky (1978). Nadharia hiyo inazungumzia mahusiano ya jamii na mazingira yanavyotoa mchango chanya katika kujifunza na kufundisha lugha. Makala hii iliongozwa na Nadharia ya Mwingiliano Jamii kwa sababu ina misingi inayokwenda sambamba na ufundishaji pamoja na ujifunzaji wa L2 kupitia wanajamii ambao ndio wazawa wa lugha.

Msingi wa kwanza umejikita katika mahusiano ya karibu kati ya mwanafunzi na watu wa jamii yake. Watu hao huwa ni msaada mkubwa katika kujifunza taaluma mbalimbali. Kwa upande mwingine kujifunza lugha L2, mwanafunzi anaweza kupata usaidizi kupitia kwa watu hao. Hao ni walimu, wazazi, marafiki, n.k. Katika utafiti huu, ni watu kwa ujumla wanaoishi kwenye mazingira ya Kiswahili. Hali hiyo hupelekea mwanafunzi kujenga imani kubwa kwa watu hao wanaomzunguka. Hivyo hurahisisha kitendo cha kujifunza.

Msingi wa pili, Vygotsky (1978) anafafanua kiwango cha uelewa, cha wanafunzi katika kujifunza kwao.

Msingi huo, unazingatia kitu cha awali alichojifunza mwanafunzi na huhitaji msaada ili aweze kujifunza taaluma au maarifa mapya. Msingi wa tatu, unahusisha nafasi ya mazingira katika kujifunza lugha. Vygotsky (1978) anafafanua kwamba mazingira ni muhimu kwa mwanafunzi katika kukamilisha malengo yake. Hii inamaanisha kwamba mazingira yana mchango mkubwa katika kujifunza na kufundisha lugha L2 ndani ya jamii.

Msingi wa kwanza na msingi wa tatu ni faafu kwa uchanganuzi wa data za utafiti huu kwa kuwa inaendana kikamilifu na dhamira ya kuchunguza namna miktadha ya kijamii inavyoathiri ujifunzaji wa Kiswahili kama L2 nchini Burundi.

Msingi wa kwanza unaolenga mahusiano ya karibu baina ya mwanafunzi na watu wa jamii, hutoa mwanga kuhusu namna ushirikiano wa kijamii unavyoweza kuchochea ukuaji wa umahiri wa lugha, hasa kupitia mazungumzo. Hali hii inaonesha kuwa ujifunzaji wa lugha haufungamani na mazingira ya darasani peke yake, bali hujengwa na kuendelezwa pia kupitia mwingiliano wa kila siku katika mazingira ya kijamii ya mwanafunzi.

Vilevile, msingi wa tatu unaozingatia nafasi ya mazingira katika ujifunzaji wa lugha, una umuhimu katika uchanganuzi wa data za utafiti huu. Msingi huo ulimwongoza mtafiti kikamilifu katika utafiti huu kwa kutia mkazo kwenye uchunguzi wa mazingira halisi yanayomzunguka mwanafunzi katika vyuo vikuu nchini Burundi. Kadhalika, Msingi huo ulimsaidia mtafiti kuelewa kama mazingira ya kijamii yana mchango katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Burundi au la.

## 3.0 MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulifanyika jijini Bujumbura nchini Burundi. Sampuli ya wasailiwa ilikuwa wanafunzi wa Kiswahili ishirini (20). Sampuli hii ni ya wanafunzi wanaoishi katika kata za Buyenzi, Bwiza, Nyakabiga na Kamenge. Kata hizo ziliteuliwa kwa sababu zina wazungumzaji wengi wa lugha ya Kiswahili (Bizimana, 2022). Utafiti huu, ulitumia usampulishaji tajwa kukusanya data za malengo ya utafiti huu. Mtoataarifa wa kwanza aliyefahamika alitumika kumtaja mtoataarifa mwingine, na mwingine naye alimtaja mwingine, na mwingine alimtaja mwingine mpaka watoataarifa wanaohitajika wakapatikana.

Mbinu ya usaili ilitumiwa kukusanya data inayolenga kupata taarifa zinazohusu kubainisha miktadha ya kujifunza Kiswahili iliopo jiji la Bujumbura, Tarafa za Mukaza na Ntahangwa. Mbinu hiyo ilitumika pia kukusanya data kuhusu mchango wa miktadha jamii katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Burundi. Data za utafiti huu zimewasilishwa kwa kutumia majedwali na grafu ili kuonesha matokeo kwa uwazi na urahisi wa kuelewa, ili kuwezesha ulinganishi wa takrimu kati ya vipengele mbalimbali vilivyofanyiwa utafiti.

## 4.0 MATOKEO YA UTAFITI

Makala hii imelenga kubainisha miktadha ya kijamii ya lugha ya Kiswahili iliyopo jijini Bujumbura na mchango wake katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama L2 kwa wanafunzi wa lugha hiyo. Kipengele hiki kinawasilisha matokeo ya utafiti yaliyokusudiwa kubainisha miktadha ya kijamii inayowazunguka wanafunzi wa Kiswahili katika maeneo teule na kuangazia namna miktadha hiyo inavyosaidia ujifunzaji wa lugha hiyo.

### 4.1 Miktadha ya Kijamii Iliyopo Jijini Bujumbura

Matokeo yanaonyesha kuwa wanafunzi wanaosoma Kiswahili katika Tarafa za Mukaza na Ntahangwa jijini Bujumbura wanapata fursa ya kuingiliana na mazingira mbalimbali ya kijamii kama vile hospitalini, vituo vya utangazaji vya redio na televisheni, familia, kanisani, marafiki, michezo, msikitini, nyumbani, sokoni na zahanati. Uwasilishaji wa miktadha hiyo umeoneshwa kwa muhtasari katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na. 1: Miktadha ya Jamii Iliyopo katika Tarafa za Mukaza na Ntahangwa Jijini Bujumbura**

| Miktadha | Buyenzi | Bwiza | Kamenge | Nyakabiga |
|---|---|---|---|---|
| 1. Hospitalini | +++ | ++ | + | - |
| 2. Redio-T.V | ++ | + | + | ++ |
| 3. Familia | +++ | +++ | ++ | + |
| 4. Kanisa | +++ | ++ | + | - |
| 5. Marafiki | +++ | +++ | ++ | + |
| 6. Michezo | +++ | +++ | +++ | +++ |
| 7. Msikitini | +++ | +++ | ++ | + |
| 8. Nyumbani | +++ | +++ | ++ | + |
| 9. Sokoni | ++ | ++ | + | - |
| 10. Zahanati | +++ | ++ | - | - |
| **Alama** | **28** | **24** | **15** | **09** |
| **Asilimia** | **93.33%** | **80 %** | **50 %** | **30%** |

**Chanzo: Data za Utafiti (2025)**

**Ufunguo:**
+++: Fursa zinatosha (Alama 3)
++: Fursa ni wastani (Alama 2)
+: Fursa ni chache (Alama 1)
-: Hakuna fursa (Hakuna Alama)

Jedwali Na.1 hapo juu linaonesha miktadha ya kijamii iliyopo katika Kata nne za Tarafa za Mukaza na Ntahangwa, Jiji la Bujumbura (Buyenzi, Bwiza, Kamenge na Nyakabiga). Uchanganuzi wa data unaonesha kuwa Buyenzi inaongoza kwa fursa nyingi za miktadha ya jamii (93.33%), ikifuatiwa na Bwiza (80%). Ndayisenga (2022) anasema kwamba Buyenzi ni Kata ambayo ina wakazi wengi wenye tamaduni tofauti. Mwanazuoni huyo anaendelea kusema kuwa Kata ya Buyenzi ni ya kwanza kwa kuwa lugha ya Kiswahili inazungumzwa sana. Eneo hilo ni kitovu cha Waswahili nchini Burundi. Bwiza pia ni eneo ambalo lina mazingira bora ya ujifunzaji wa Kiswahili kama L2 katika Jiji la Bujumbura. Kamenge ina kiwango cha wastani wa fursa (50%), wakati Nyakabiga inaonekana kuwa na fursa chache (30%), na ina viashiria vya ukosefu wa miktadha muhimu kama vile kwa mganga, redio-televisheni na zahanati.

Data zinaonesha kwamba wanafunzi wa Kiswahili wanaoishi Buyenzi na Bwiza wako katika mazingira yanayowezesha mazoezi ya mara kwa mara ya lugha, jambo ambalo linaweza kuwa na mchango katika upataji wa umahiri wa lugha ya Kiswahili. Nyakabiga kwa upande mwingine, inahitaji mikakati ya ziada ili kuimarisha miktadha ya kijamii inayochochea ujifunzaji wa Kiswahili kama L2 nchini Burundi.

### 4.2 Mchango wa Miktadha ya Jamii katika Ujifunzaji Lugha ya Kiswahili

Sehemu hii ya Makala inajadili mchango wa miktadha ya kijamii kwa wanafunzi wa Kiswahili kama L2 Tarafa za Mukaza na Ntahangwa, jijini Bujumbura. Matokeo yanaonesha kuwa mazingira ya kijamii yanatoa fursa ya moja kwa moja kwa wanafunzi kuingiza msamiati mpya, kukuza stadi za kusikiliza na kuzungumza, kuimarisha umilisi wa utamaduni na kumiliki fasihi ya jamii. Michango hiyo inaelezwa mmoja baada ya mwingine kwenye sehemu zinazofuata.

#### 4.2.1 Kuingiza Msamiati Mpya wa Kiswahili

Miktadha ya kijamii ina nafasi muhimu katika uendelezaji wa lugha kwa wanafunzi wa lugha ya pili. Kupitia mwingiliano wa kila siku katika jamii, wanafunzi wanapata fursa ya kukutana na maneno mapya yanayotumika katika mazingira halisi. Sehemu hii inaonesha jinsi miktadha ya kijamii inavyorahisisha upataji wa msamiati mpya. Data zimeoneshwa katika jedwali na grafu ifatavyo:


**Jedwali Na. 2: Miktadha Inayochangia Kuingiza Msamiati Mpya wa Kiswahili**

| | Mazungumzo maalumu | Redio na Televisheni | Mazungumzo ya kawaida | Michezo na marafiki |
|---|---|---|---|---|
| Wasailiwa | 4 | 6 | 4 | 6 |
| Asilimia | 20 | 30 | 20 | 30 |

**Chanzo: Data za Utafiti (2025)**

Takwimu zilizooneshwa kwenye jedwali 2 zimeoneshwa pia kwa njia ya kielelezo 1 kama ifuatavyo:

**Kielelezo Na. 1: Miktadha Inayochangia Kuingiza Msamiati Mpya wa Kiswahili**




**Chanzo: Data za Utafiti (2025)**

Matokeo yamebainisha kuwa wanafunzi wanaoishi katika miktadha ya kijamii wanapata nafasi ya kushiriki katika mazungumzo ya mada mbalimbali. Wanafunzi wanne (4) sawa na asilimia 20 walilipoti kuwa wanapata msamiati mpya katika mazungumzo maalumu kama vile mazungumzo yanayohusu siasa, utawala, huzuni, faraja, n.k. Kwa upande mwingine, lugha ya sheria ina sifa ya kutumia sentensi ndefu, marudio ya maneno na msamiati maalumu wa kisheria. Washiriki sita (6) sawa na asilimia 30 walieleza kuwa wanasikiliza vipindi vya redio na televisheni vya Taifa vinavyoendeshwa kwa Kiswahili.Wanaripoti kuwa, vipindi vya redio na televisheni kwa Kiswahili vinawasaidia kujifunza msamiati mpya kwa kuonyesha maneno katika miktadha halisi ya mazungumzo. Kupitia marudio ya maneno na picha zinazohusiana, wanafunzi wanapata fursa ya kuelewana na kukumbuka maneno mapya. Washiriki waliendelea kusema kwamba vipindi hivyo hujumuisha nyimbo mbalimbali, hasa zile zinazoonyeshwa kwenye kipindi maarufu Zinazopendwa cha televisheni ya taifa. Wasanii wa Burundi kama Big Fizzo, Sat B, B – Face na Natacha, huimba kwa Kiswahili na nyimbo zao hutumika kama nyenzo ya kukuza uwezo wa kusikiliza kwa wanafunzi wa Kiswahili. Wasailiwa walieleza kuwa nyimbo hizo huwa na misamiati amao huweza kueleweka na kutumiwa kwa urahisi kama katika nyimbo Jambo Bwana, Anapenda Vitu vya Bei Ghali, Badilisha, na nyinginezo. Pia katika makanisa, nyimbo kama Toa Sadaka na Utukuzwe Bwana huimbwa mara kwa mara. Jambo hilo huwasaidia kujifunza maneno mpya. Kwa hiyo, nyimbo huchangia hamasa na kuongeza misamiati kwa wanafunzi wa Kiswahili.

Zaidi ya hapo, wasailiwa wanne (4) sawa na asilimia 20 walijulisha kwamba wanapata msamiati kupitia mazungumzo ya kawaida kama mazungumzo ya nyumbani, kwa majirani, sokoni, hasa soko la Ruvumera (Buyenzi) na soko la Jabe (Bwiza), ambako huwasiliana na wafanyabiashara kwa lugha ya

Kiswahili. Hali hii inawasaidia kujifunza Kiswahili kama lugha ya matumizi ya kila sikuna biashara.

Wasailiwa sita (6) sawa na asilimia 30 walisema kwamba wanapata marafiki wengi kupitia kuzungumza Kiswahili. Urafiki hueleza zaidi kwa maneno kama vile shughuli za kawaida. Urafiki wao pia hutoa fursa ya kucheza na kufanya maigizo ya binafsi. Mchezo unaotoa fursa hasa ya kusikiliza na kuzungumza mpira wa miguu. Vijana wa Buyenzi jijini Bujumbura wanapenda sana mchezo huo. Hivyo, ni fursa kwa mjifunzaji wa Kiswahili kama L2 kuingiza msamiati mpya kutoka kwa marafiki zake. Kukuza kiwango cha msamiati, ni jambo la msingi katika kujifunza L2 au ya kigeni (Alqahtani, 2015) kwa kuwa ndio msingi mkuu wa mjifunzaji kujifunza lugha inayohusika. Ili mwanafunzi aweze kutumia lugha vizuri na kuweza kuwasiliana na watumiaji wa lugha hiyo, hana budi kukuza kiwango chake cha misamiati. Kiwango hicho huwasaidia wanafunzi kuimarisha stadi zote za ujifunzaji L2. Mjifunzaji huweza kuimarisha stadi ya kusikiliza kwa kuwa anaelewa mazungumzo kutokana na kuwa na uelewa mpana wa msamiati.

#### 4.2.2 Kukuza Stadi za Kusikiliza na Kuzungumza Lugha ya Kiswahili

Kukuza stadi za kusikiliza na kuzungumza ni muhimu katika mchakato wa kujifunza lugha. Stadi hizi huimarisha mawasiliano ya mdomo na uelewa wa lugha katika miktadha ya kila siku. Nyimbo za Kiswahili zinazopiwa kwenye redio na televisheni zinatoa fursa muhimu ya kujifunza. Hebu tutazame jedwali lifuatalo kwa udhihirisho zaidi.


**Jedwali Na. 3: Fursa za Kusikiliza na Kuzungumza Lugha ya Kiswahili**

| | Redio na Televisheni | Msikitini | Mazungumzo ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Wasailiwa | 11 | 3 | 6 |
| Asilimia | 55 | 15 | 30 |

**Chanzo: Data za Utafiti (2025)**

Takwimu zilizooneshwa kwenye jedwali 3 zimeonyeshwa pia kwa njia ya kielelezo 2 kama ifuatayo:

**Kielelezo Na. 2 : Fursa za Kusikiliza na Kuzungumza Lugha ya Kiswahili**




**Chanzo: Data za Utafiti (2025)**

Wanafunzi kumi na moja (11) sawa na (55%) waliripoti kuwa wanasikiliza nyimbo na vipindi vya Kiswahili hasa vile vya watoto, ambavyo huwasaidia kukuza stadi ya kusikiliza. Hii inaonesha kuwa, ingizo la lugha kupitia mazingira ya kijamii na burudani huongeza ufanisi katika ujifunzaji wa lugha. Wanafunzi wa lugha ya Kiswahili kama L2 hupata fursa nyingi za kujifunza kupitia usikilizaji wa nyimbo, vipindi vya redio na mazungumzo ya kila siku. Wasailiwa wa utafiti huu wamesema kwamba, wanapokuwa wanasikiliza muziki wa Kiswahili, wanazingatia kwa makini mashairi, melodia na mdundo wa nyimbo hizo. Hali hii huwasaidia kujifunza msamiati mpya na kuwapa uwezo wa kuitumia lugha hiyo katika mazungumzo. Kwa hiyo, nyimbo ni zana bora ya kukuza msamiati na stadi ya kusikiliza, huku ikiwawezesha pia kutambua sauti na lafudhi mbalimbali za Kiswahili. Aidha, wasailiwa waliendelea kusema kwamba wanasikiliza mechi za mpira wa miguu kupitia redio Rema FM. Baada ya kusikiliza, hushiriki katika majadiliano ya kandanda ambayo huwapa nafasi ya kuzungumza Kiswahili na kutoa maoni kati yao.

Vilevile, wasailiwa watatu (3) sawa na (15 %) Waislamu walieleza kuwa wanasikiliza hotuba na mafundisho msikitini. Jambo hilo linawawezesha kuimarisha stadi zao za kusikiliza na kuzungumza lugha ya Kiswahili inayotumika kwenye mahubiri hayo. Mazingira haya ya kijamii yanakuwa msaada wa maendeleo ya umahiri wa lugha ya Kiswahili.

Kadhalika, washiriki sita (6) sawa na (30%) wanaripoti kuwa mjifunzaji wa lugha anayeishi katika miktadha ya jamii hukuzwa katika stadi za kusikiliza na kuzungumza lugha anayojifunza. Wanaeleza kwamba wanapata fursa ya kushiriki kikamilifu katika mazungumzo ya kawaida ili kuboresha uwezo wao wa kuboresha stadi za kusikiliza na kuzungumza ambazo ni stadi za msingi katika ujifunzaji wa lugha na huchangia moja kwa moja katika maendeleo ya kitaaluma darasani. (Donaldson, 2012). Hata hivyo, mwanafunzi anahitaji kuwa na motisha inayomvutia kushiriki katika mazungumzo hayo.

**4.2.3 Kuimarisha Umilisi wa Utamaduni**

Miktadha ya kijamii ni nyenzo muhimu katika ujifunzaji wa lugha hasa katika kukuza umahiri wa kuelewa na kuimarisha utamaduni wa jamii husika. Katika muktadha huu wasailiwa wa utafiti huu, walionesha kwamba mwanafunzi anayeishi katika mazingira ya Kiswahili, hupata fursa ya kujifunza zaidi ya maneno ya lugha hiyo, kwa kuhusisha mila, desturi na mitazamo ya jamii inayozunguka lugha hiyo. Jedwali na grafu inaonesha matokeo yafuatayo ya utafiti huu:


**Jedwali Na. 4: Fursa za Kuimarisha Umilisi wa Utamaduni**

| | Mapishi | Sherehe | Mavazi |
|---|---|---|---|
| Wasailiwa | 12 | 6 | 2 |
| Asilimia | 60 | 30 | 10 |

**Chanzo: Data za Utafiti (2025)**

Takwimu zilizooneshwa kwenye jedwali 4 zimeoneshwa pia kwa njia ya kielelezo 3 kama ifuatavyo:

**Kielelezo Na. 3 : Fursa za Kuimarisha Utamaduni**




**Chanzo: Data za Utafiti (2025)**

Wasailiwa kumi na wawili (12) sawa na (60%) hasa wasichana walisema kwamba wanajifunza utamaduni jinsi ya kupika pilau. Wawili wameishi jijini Bujumbura kipindi cha miaka miwili, watatu nao miaka mitatu. Tayari wanajua jinsi ya kuandaa na kupika Pilau la nyama ya ng'ombe au ya kuku nyumbani kwao. Walisema kwamba pilau ni chakula maarufu katika jamii nyingi za Afrika Mashariki, hasa miongoni mwa waswahili. Ni chakula kinachoonesha utamaduni wa upishi wa Kiswahili, kikiashiria mchanganyiko wa ladha, harufu na mapishi yenye sili ya Kiarabu na Bara Hindi, yaliyochanganyika na ladha za kiafrika. Utamaduni wa pilau huu ni ufuatao: Kwanza, hupikwa kwenye hafla kama harusi, Idd, misiba, au mikutano ya kifamilia. Pili, ni ishara ya ukarimu na sherehe. Tatu, wanafunzi wa Kiswahili wanaweza kujifunza si tu maneno ya mapishi, bali pia mila za jamii kupitia vyakula kama pilau.

Aidha, wasailiwa sita (6) sawa na (30 %) walisema kwamba walihudhuria sherehe za harusi. Nyimbo zinazoimbwa kwenye harusi zinawavutia sana. Walitoa mfano wa wimbo wa Kajanine, Mapenzi ya Hisia, ambayo huonesha kuwa mapenzi ya kweli hutoka moyoni na si kwa mali, ikiwafundisha wanafunzi kuhusu thamani ya hisia katika jamii ya Burundi na Afrika nzima. Wimbo mwingine ni wa Kidumu (Kibuganizo), Umeniweza, ambao huonesha uamilifu na ushindi wa mapenzi ya dhati, jambo linalooonesha umuhimu wa kuvumiliana katika ndoa.

Isitoshe, wasailiwa wawili (2) sawa na (10%) walilipoti kuwa mavasi ni muhimu katika utambulisho wa utamaduni wa jamii husika. Hapa walieleza kwamba, mavazi kama kanga, kitenge na kanzu kwa wanaume hubeba ujumbe wa jamii. Kanga inavaliwa na wanawake, mara nyingi huwa na maandishi kama methali au misemo yenye mafunzo na ikawa njia ya mawasiliano na jamii. Kitenge kinavaliwa na wanaume na wanawake hasa kwenye sherehe. Kinaweza kuwa na maandishi ya Kiswahili yanayovutia wasomaji. Kanzu inayovaliwa na wanaume inaonyesha utamaduni wa kiislamu unaotawala Tarafani Mukaza, Kata za Buyenzi na Bwiza jijini Bujumbura, nchini Burundi. Wanafunzi wa Kiswahili walioshiriki katika utafiti huu, waliendelea kusema kwamba wanapotazama mavazi yenye maandishi ya Kiswahili, siyo tu kupanua msamiati bali pia wanajifunza namna lugha inavyohusiana na utamaduni, mathalani namna methali kwenye kanga zinavyotumiwa kufikisha ujumbe kwa jamii. Hivyo, mavazi yanachangia katika kuelewa muktadha wa kijamii wa lugha ya Kiswahili.

Kulingana na data za wasailiwa, miktadha ya kijamii huwasaidia wanafunzi kuelewa lugha na utamaduni wa jamii, kwa kuwa lugha ni chombo muhimu cha mawasiliano kinachoakisi hisia, maadili na imani za kitamaduni. Kupitia mwingiliano wa kila siku, wanafunzi hujifunza msamiati, semi na tamaduni tofauti ambazo huwajengea uelewa mpana wa jamii na

kusaidia kuhifadhi utambulisho wa kiutamaduni. Kama mazingira ya kijamii yanavyounda jinsi watoto wanavyojifunza lugha, lugha yenyewe inakuwa njia ya kujifunza kuhusu maisha ya kijamii na kiutamaduni. Wasailiwa wanasema kwamba wanazoea mazingira yao hasa kutokana na matumizi ya lugha ambao inatumiwa na watu wengi kwenye jamii husika. Kuna mtagusano wa muda mrefu kati ya wanafunzi na jamii ya Kata za Buyenzi, Bwiza, Jabe, Kamenge na Nyakabiga. Hali hiyo hupelekea kuathiriwa katika matumizi ya Kiswahili ndani ya jamii hiyo na humwezesha mwanafunzi kuimarisha umilisi wa utamaduni wa mahali anapoishi.

#### 4.2.4 Kumiliki Maarifa ya Fasihi

Uhusiano kati ya lugha na fasihi simulizi ni karibu sana na unategemeana. Lugha ni chombo cha msingi kinachotumika kuunda na kuwasilisha fasihi simulizi. Bila lugha, haiwezekani kuwa na fasihi simulizi. Uhusiano wa fasihi na jamii unabainishwa na lugha inayoifanya itofautiane na sanaa nyinginezo ni matumizi ya lugha na lugha ni sifa imhusuyo binadamu na si wanyama. Binadamu ni wanajamii na mwanafasihi ni mwanajamii pia. Lugha aitumiayo binadamu huwa ni lugha ya jamii fulani. Kama lugha itumiwayo na binadamu ni lugha ya jamii fulani, mwanafasihi naye ni binadamu na ni mwanajamii katika jamii fulani, basi bila ya shaka msanii hutumia lugha ya jamii au binadamu hulenga kuwasiliana miongoni mwao na lengo kuu la kuwasiliana huwa ni kupata ujumbe maalumu. Kwa mantiki hiyo basi, lugha ya fasihi ni zao la jamii. Pia, lugha hutumika kuunda mitindo ya kipekee wa hadithi, kama vile ucheshi, huzuni, au mafunzo. Hebu tueleze kidogo kuhusu fasihi simulizi na andishi katika miktadha ya matumizi ya lugha.

##### 4.2.4.1 Fasihi Simulizi

Kwa mujibu wa Matei (2010), fasihi simulizi hubuniwa na kuhifadhiwa akilini. Anaendelea kudai kuwa fasihi simulizi huwasilishwa na kusambazwa kwa masimulizi, mazungumzo ya kisanaa, kuimba, kughani, kuigiza na kukariri kwa hadhira hai. Naye Mulokozi (2017) anadai kuwa fasihi simulizi ni dhana inayotumika kueleza fasihi itolewayo kwa mdomo bila kuandikwa. BAKITA (2017) linafasili kuwa fasihi simulizi ni aina ya fasihi inayotolewa kwa njia ya matamshi kama vile hadithi, ngojera, vitendawili, na huhifadhiwa na kurithishwa kutoka kizazi kimoja kwenda kingine kwa njia ya mdomo. Kwa jumla, fasihi simulizi ni sanaa inayotungwa au kubuniwa kichwani na kuwasilishwa kwa hadhira kwa njia ya mdomo na vitendo bila kutumia maandishi; yaani katika hali ya kuimba, kusimulia, kuigizana kughani. Lugha ya Kiswahili hutumika kuhifadhi na kusambaza fasihi simulizi katika miktadha mbalimbali iliyopo jijini Bujumbura.

Wasailiwa ishirini (20) sawa na (100%) walijulisha kwamba wanapata vipera vya semi za fasihi simulizi (kwa kiwango tofauti) katika jamii kama vile hadithi, methali, misemo, nahau, mashairi na vitendawili kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na. 5 : Fursa za Kupata Maarifa ya Fasihi Simulizi**

| Wasailiwa | Methali | Hadithi | Misemo | Nahau | Shairi | Vitendawili |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | - | + | + | + | - | + |
| 2. | - | - | + | + | - | + |
| 3. | - | - | + | + | - | + |
| 4. | + | + | + | + | - | + |
| 5. | + | - | + | + | - | + |
| 6. | + | - | - | - | - | + |
| 7. | - | - | + | + | + | + |
| 8. | - | - | + | + | + | + |
| 9. | - | | - | - | - | + |
| 10. | - | + | + | + | - | + |
| 11. | + | - | - | - | - | + |
| 12. | + | + | - | - | - | - |
| 13. | + | + | - | - | - | + |
| 14. | - | - | - | - | - | + |
| 15. | - | - | - | - | - | + |
| 16. | + | + | - | - | + | + |
| 17. | - | - | + | + | + | - |
| 18. | + | + | + | + | + | + |
| 19. | + | | + | + | - | + |
| 20. | + | - | + | + | - | + |
| Alama | 10 | 7 | 12 | 12 | 4 | 18 |
| % | 50% | 35% | 60% | 60% | 20% | 90% |

**Chanzo: Data za Utafiti (2025)**

**Ufunguo:**
+: (Alama 1)
-: (Hakuna Alama)

Takwimu hizi zinaonesha matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi katika jamii miongoni mwa wanafunzi ishirini (20) wa Kiswahili. Walisema kwamba, wanapata vipengele hivyo vikitolewa nyumbani kwao na kwenye vipindi vya redio na televisheni ya Taifa na redio Rema.F.M na mara chache kutoka kwa marafiki zao. Inaonekana kuwa, vitendawili (90%) na misemo na nahau (60%) hutumika sana, ikimaanisha kuwa wanafunzi wanapata fursa nzuri ya kujifunza Kiswahili kupitia vipengele hivyo. Methali (50%) na hadithi (35%) zinatumika kwa kiwango cha kati, huku mashairi yakitumiwa kwa kiwango cha chini zaidi sawa na (20%).

Uchunguzi huu umeonesha kuwa wanafunzi wa Kiswahili wanaoishi katika mazingira ya lugha hiyo wananufaika kwa kiwango kikubwa na mazingira yao ya kijamii kupitia fasihi simulizi. Wasailiwa wanaeleza vipengele vya jamii kama vile hadithi za jadi, nyimbo, vitendawili, methali na nahau vinawawezesha kujifunza Kiswahili kwa urahisi na kwa njia hai. Hii ni kwa sababu vipengele hivi hupatikana jijini Bujumbura, Tarafa za Mukaza na Ntahangwa, nyumbani, kanisani, msikitini na hata kupitia vyombo vya habari kama redio ya Taifa na redio Isanganiro na redio Culture. Miktadha hiyo ya kijamii huwasaidia wanafunzi kuelewa lugha katika matumizi yake halisi.

Wasailiwa walisema kwamba vitendawili, misemo na nahau ni njia zenye nguvu zaidi kukuza umahiri wa lugha katika miktadha ya kijamii. Hata hivyo, matumizi hafifu ya mashairi yanaweza kudokeza ukosefu wa nyenzo au fursa kwa wanafunzi kutumia aina hii ya fasihi katika ujifunzaji wao wa Kiswahili. Kwa jumla, data zinaonesha kuwa wanafunzi hupata fursa zaidi ya kujifunza Kiswahili kupitia vipengele vya fasihi simulizi vinavyojitokeza katika mazingira ya kawaida kama vile

vitendawili, misemo na nahau. Ni vema kuimarisha matumizi ya vipengele vingine kama mashairi na hadithi kwa kuwa navyo vinaweza kuwa na mchango katika kukuza utamaduni na umahiri wa lugha.

#### 4.2.4.2 Fasihi Andishi

Fasihi andishi ni aina ya sanaa ambayo hutumia maneno yanayoandikwa kupitisha ujumbe. Aidha, ni sanaa inayotolewa kwa njia ya maandishi. Kwa bahati mbaya, wasailiwa wote walisema kwamba hawana fursa ya kuimudu lugha ya Kiswahili kupitia fasihi andishi katika miktadha ya kijamii ya Jiji la Bujumbura. Jedwali na grafu ifuatayo inaonesha matokeo ya utafiti huu.


**Jedwali Na. 6: Hakuna Fursa za Kupata Maarifa Kupitia Fasihi Andishi**

| | Fasihi Simulizi | Fasihi Andishi |
|---|---|---|
| Wasailiwa | 20 | 0 |
| Asilimia | 100 | 0 |

**Chanzo: Data za Utafiti (2025)**

Takwimu zilizooneshwa kwenye jedwali 6 zimeonyeshwa pia kwa njia ya kielelezo 4 kama ifuatayo:

**Kielelezo Na. 4: Hakuna Fursa za Kupata Maarifa Kupitia Fasihi Andishi**




**Chanzo: Data za Utafiti (2025)**

Wasailiwa wote ishirini (20) sawa na (100%) wanalalamikia kwamba kuna ukosefu wa fasihi andishi ya Kiswahili. Katika kuelezea suala hilo walisema kwamba, hakuna vitabu vya riwaya, tamthilia, mashairi au kazi nyingine za kifasihi zilizoandikwa au kusambazwa kwa Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa jijini Bujumbura. Hali hii inawanyima nafasi ya kukuza stadi za kusoma na kuandika. Kadhalika, walimjulisha mtafiti kwamba maktaba iliyopo Chuo Kikuu cha Ualimu ENS Burundi na Chuo Kikuu cha Burundi, Taasisi ya IPA (Institut Pedagogique Appliqée), zina vifaa vya fasihi andishi vichache ila hawaruhusiwi kuingia maktabani. Mwanafunzi hatakuwa na uwezo wa kuelewa na kuimudu lugha kwa undani zaidi. Kwa hiyo, kuna haja ya kuhimiza upatikanaji wa vitabu na vifaa vingine vya kifasihi ya Kiswahili katika shule, maktaba na jamii kwa jumla ili kuwasaidia wanafunzi kuimarisha stadi zao kupitia fasihi zote mbili: fasihi simulizi na andishi pia.

## 5.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho:** Kwa mtazamo wa kitaaluma, ujifunzaji wa lugha unaofanikisha uelewa wa kina ni ule unaojengwa katika miktadha halisi ya kijamii inayowagusa wanafunzi moja kwa moja. Wanafunzi wanapoingia darasani wakiwa na maarifa ya awali waliyojipatia kupitia mawasiliano katika miktadha ya kijamii hasa kutoka kwa wenyeji, huleta mada halisi, zenye uhai na mvuto kwao binafsi. Hali hii huibua mijadala ya kina darasani na kuchochea ushiriki hai wa wanafunzi. Ushiriki huo huonekana zaidi kwa wanafunzi wanaoishi katika mazingira ya Kiswahili hasa katika familia za wenyeji, ambao huibua hoja mbalimbali na kutumia miundo ya lugha kwa njia bunifu, kama ilivyobainishwa na msailiwa mmoja aliyeshiriki katika utafiti huu.

Miktadha ya jamii iliyopo jijini Bujumbura iliyobainika ni kama vile hospitalini, vituo vya utangazaji vya redio na televisheni, familia, kanisani, marafiki, michezo, msikitini, nyumbani, sokoni na zahanati. Ilionekana kwamba miktadha ya kijamii hiyo huchangia kwa kiasi kikubwa kwa wanafunzi wa Kiswahili wanaoishi katika miktadha hiyo. Inawasaidia kupata msamiati mpya, kukuza stadi za kusikiliza na kuzungumza, kujua utamaduni na fasihi simulizi ya jamii. Hivyo, kuingiza msamiati mpya hurahisisha mawasiliano na mijadala baina ya wazungumzaji wa lugha hiyo katika mazingira mbalimbali. Wanafunzi wanaoishi katika miktadha ya kijamii hujihusisha na mazungumzo mafupi yenye kubeba maana. Hali hii inawezesha kubadilishana mawazo na kukuza umahiri wa lugha kwa njia ya asili. Katika taaluma ya upataji ya L2, wanafunzi huangazia si tu hatua za ujifunzaji wa lugha, bali pia mazingira ya kijamii ambamo lugha hiyo hutumika na kujifunzwa.

**Mapendekezo:** Mtafiti anapendekeza mosi, Wizara ya Elimu ya Burundi iandae mitaala ya Kiswahili inayojumuisha matumizi ya lugha katika miktadha halisi ya kijamii ili kuleta uhusiano kati ya mazingira ya wanafunzi na maudhui ya somo. Pili, anapendekeza kuwa matumizi ya vyombo vya habari vyote nchini Burundi, viandae vipindi katika lugha ya Kiswahili na vitumike kama nyenzo za kujifunzia lugha ya Kiswahili. Tatu, anapendekeza utafiti fuatizi ufanyike ili kubaini changamoto zinazokwamisha matumizi ya miktadha ya kijamii katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama L2 kwa wanafunzi wa shule za sekondari jijini Bujumbura. Mapendekezo hayo yakitekelezwa, lugha ya Kiswahili itakuwa hai na yenye maana kwa wanafunzi nje ya darasa. Aidha yatarahisisha ushirikiano wa wanafunzi nje ya darasa pamoja na kutambua kutumia miktadha ya kijamii kama mbinu rasmi ya kukuza na kuendeleza kujifunza Kiswahili kama L2.

## 6.0 MAREJELEO


Alqahtani, M. (2015). The importance of vocabulary in language learning and how to be taught. *International Journal of Teaching and Education, 3*(3), 21–34.

BAKITA. (2017). *Kamusi kuu ya Kiswahili* (Toleo la pili). Longhorn Publishers.

Bizimana, J. (2022). *Athari za kimofofonolojia za lugha ya Kirundi katika ujifunzaji wa Kiswahili kama L2 kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi* (Tasnifu ya umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Donaldson, R. M. (2012). *Teaching foreign language conversation: A conversation norms approach* (Unpublished doctoral dissertation). California State University, Chico.

Ellis, R. (2008). *The study of second language acquisition* (2nd ed.). Oxford University Press.

Gass, S. M. (1997). *Input, interaction, and the second language learner*. Lawrence Erlbaum Associates.

Labov, W. (2000). *The social stratification of English in New York City*. Cambridge University Press.

Long, M. H. (1996). The role of the linguistic environment in second language acquisition.

Matei, M. (2010). Discourse markers as functional elements. *Bulletin of the Transilvania University of Brașov, 3*(1), 119–126.

Mulokozi, M. M. (2017). *Tanzu za fasihi simulizi*. TUKI.

Ndayisenga, C. (2022). *Hali ya ufundishaji wa Kiswahili katika vyuo vikuu nchini Burundi* (Tasnifu ya uzamili, haijachapishwa). Ecole Normale Supérieure, Bujumbura.

Stern, H. H. (1983). *Fundamental concepts of language teaching*. Oxford University Press.
Vygotsky, L. S. (1978). *Mind in society: The development of higher psychological processes*. Harvard University Press.
Wardhaugh, R. (2006). *An introduction to sociolinguistics* (5th ed.). Blackwell Publishing.